Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Uongozi wa kisekula wadunisha Madrasa zetu kiasi hiki!

**HABARI NA MAONI**
Muislamu Anayedaiwa Kuwa 'Gaidi' Hastahili Kuachiliwa na Mahakama chini ya Tawala za Kisekula!

**TOLEO JIPYA**
Kuanguka kwa Dini Katika Mfumo wa Kisekula sio Ajabu, ni Jambo Lakutarajiwa

**JIBU LA SWALI**
Mzozo Kati ya Uturuki na Ugiriki katika Eneo la Mashariki mwa Mediterranea



# Ubaguzi wa Serikali dhidi ya Uislamu na Waislamu

# Kufungwa kwa Madrasa Nchini Kenya: Ubaguzi wa Serikali dhidi ya Uislamu na Waislamu

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

Mnamo Jumatatu, 28 Septemba 2020 Rais Uhuru Kenyatta alitangaza kufunguliwa kwa baa na mikahawa na kuruhusiwa kuuza pombe (The Standard, 28/09/2020)! Hivi sasa wazazi nchini wako mbioni kutimiza masharti muhimu ya kuhakikisha kuwa watoto wao wamerudi shule kwa kuitikia agizo la serikali la kufunguliwa kwa shule kwa awamu kuanzia mnamo Jumatatu, 12 Oktoba 2020 (The Star, 06/10/2020). Kwa kuongezea, viongozi wa kisiasa wanavutana katika kampeni za kisiasa ambazo zinatishia usalama wa taifa kiasi kwamba mnamo Jumamosi; Rais Uhuru aliongoza Maombi ya Kitaifa eti kuliombea taifa liweze kuhimili changamoto za kisiasa, kiuchumi na kijamii zinazolikumba taifa!

Inatia wasiwasi kuona kwamba madrasa zinataabika na hazina anayeangazia matatizo yao tangu kufungwa kwao mnamo Machi 2020 kwa kisingizio cha kupambana na janga la Covid-19. Wanafunzi, walimu na wazazi Waislamu wanapata shida kwa sababu kusoma kumesitishwa kabisa na wamebakia njia panda wasijue la kufanya kusuluhisha janga hilo. Wale wanaoitwa viongozi wa kidini na kisiasa Waislamu wamenyamaza kimya na wanafuata na kujifunga na maagizo ya serikali kama ambaye ni bendera zinaelekezwa na upepo!

Hali hii sio ya sadfa badala yake ndio ukweli wa uhalisia wa namna tawala za kisekula za kirasilimali zinavyoendesha mambo yake. Kiuhakika, Kenya ni dola ya kisekula na vipaombele vyake vinasukumwa na usekula. Kwa hiyo, madrasa ni taasisi za Waislamu ambazo zinadaiwa na tawala za kisekula ikiwemo Kenya kuwa ndio vituo vya 'upenyezaji wa misimamo mikali.' Hivyo basi, Covid-19 imetoa fursa kwa tawala hizi kuzidhibiti uwepo wake na ndio sababu serikali ya Kenya imenyamazia kimakusudi suala la kufunguliwa kwa madrasa ilhali inakwenda mbio kuhakikisha baa, mikahawa na shule zinafunguliwa!

Ni unafiki kwa serikali hiyo hiyo kuwaita viongozi wa dini wakijumuisha wale wanaodai ni viongozi wa Waislamu katika yale yanayoitwa 'Maombi ya Kitaifa' na kisha rais anaomba msamaha pasi na kuelezea khaswa ni nani aliyemkosea. Uislamu na Waislamu wanabaguliwa na kukandamizwa kwa kisingizio cha vita dhidi ya ugaidi na misimamo mikali. Na ukimya huu wa kimakusudi katika kutofunguliwa kwa madrasa ni sehemu ya muendelezo wa ubaguzi wa dola ya kisekula ya Kenya dhidi ya Uislamu na Waislamu. Kwa kuongezea, wale wanaodai kuwa ni watetezi wa haki za kibinadamu wameungana na asasi za serikali juu ya hili!

Uislamu na Waislamu wanajipata katika hali hii kwa sababu wao ni mayatima wasiokuwa na mlinzi na ngao ya kuwalinda kutoka kwa maadui wa Uislamu na Waislamu. Kukosekana kwa Dola ya Kiislamu ya Khilafah ndio chanzo cha hali hii ya kutamausha ya Uislamu na Waislamu sio tu nchini Kenya bali duniani kote. Kuvunjwa kwa Khilafah mnamo 28 Rajab 1342 H sawia na 3 Machi 1924 M kwa mikono ya usaliti ya Mustafa Kamal aliyelaaniwa akiongozwa na dola kuu duniani wakati huo Wamagharibi wakoloni, Uingereza na Ufaransa ndio mwanzo wa matatizo yetu. Hivyo basi, tunaongozwa na muongozo wa Ukafiri (itikadi ya kisekula/ilmaniyya) na Makafiri (wakati huo Uingereza na sasa Amerika na washirika wake). Ama kuhusu njia ya kutatua suala la madrasa; ni kuchukua hatua mbili muhimu:

**Kwanza,** mchakato wa muda mfupi – Waislamu nchini Kenya lazima waungane na kudai kufunguliwa kwa madrasa zao pasi na masharti. Ili kufaulisha mchakato huu lazima wawe imara na kuepuka sintofahamu zao duni za muda mrefu ambazo zimekuzwa kimakusudi na maadui wa Uislamu na Waislamu ili kuwagawanya na kuwakoloni daima. Katika kipindi chote cha mchakato huu lazima waunganishwe na 'La Ilaha Ila Allah' pekee na wajiepushe na aina yoyote ya vurugu au nguvu. Hatimaye ni kuchua hatua ifuatayo.

**Pili,** mchakato msingi na mpana – Waislamu nchini Kenya lazima waunge juhudi zinazoongozwa na chama cha Kiislamu cha Hizb ut Tahrir 'chama cha ukombozi.' Chama cha Kiislamu kinachosimama juu ya ukweli, hakiudanganyi Ummah wa Waislamu na wanadamu kwa ujumla na HAKITUMII vurugu wala nguvu katika kufikia lengo lake la kurudisha maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha Dola ya Kiislamu ya Khilafah kwa njia ya Utume. Ni kupitia mchakato huu PEKEE ndipo wanadamu watakombolewa kiukamilifu kutoka katika minyororo ya mfumo batili wa kisekula wa kirasilimali na nidhamu zake zenye sumu ambazo zinaleta maangamivu duniani kote. Waislamu na wasiokuwa Waislamu watafurahi na kupata ustawi, amani na utulivu wa kweli ambao wameukosa na badala yake wamekuwa wakizama ndani ya moto wa kudumu wa kisekula! Mwenyezi Mungu (swt) asema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَنصُرُوا اللَّهَ يَنصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ

"Enyi mlio amini! Mkimnusuru Mwenyezi Mungu naye atakunusuruni na ataithibitisha miguu yenu."
[Muhammad 47: 7].

 Email: info@uqab.or.ke

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

﴿ وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ مِنكُمْ وَعَمِلُوا۟ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِى ٱلْأَرْضِ كَمَا ٱسْتَخْلَفَ
ٱلَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ ٱلَّذِى ٱرْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ
يَعْبُدُونَنِى لَا يُشْرِكُونَ بِى شَيْـًۭٔا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُو۟لَٰٓئِكَ هُمُ ٱلْفَٰسِقُونَ ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 03/1442 Jumanne, 12 Safar 1442 H 29/09/2020 M

# Uongozi wa kisekula wadunisha Madrasa zetu kiasi hiki!

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Wakati tunapomshukuru MwenyeziMungu (swt) kwa kupungua maambukizi ya Covid -19 humu nchini, wakati huohuo tunasikitishwa na hatua ya serikali ya kufungua vilabu vya vileo huku Madrasa za Kiislamu kutogusiwa kamwe. Suala hili la kufungua Madrasa pia halijahusishwa kwenye mjadala wa ufunguzi wa shule unaofukuta baina ya wazazi, wizara ya elimu na ile ya afya. Huu ni ubaguzi wa wazi usiofaa kwani ni jukumu la serikali kusimamia maslahi ya raia wake wote kwa ujumla.Licha ya kufahamu kwetu hali duni ya Madrasa zetu leo ambayo kwa hakika imetokamana na kukosekanwa utawala wa Khilafah,lakini tunatambua dori muhimu ya vyuo hivi katika kuhifadhi shakhsiya za Kiislamu kwa wototo wetu.

Tawala za Kisekular siku zote hupambika na sifa mbili zenye kukinzana kwa wakati mmoja, Huku Madrasa zikiwa bado wamezifunga kwa kohofia maambukizi, viongozi wake wanaonekana kwenye mikutano wakihubiri porojo zao kisiasa mbele ya halaiki huku wakikiuka masharti yote ya kujikinga na maambukizi. Je; ndani ya Madrasa ndio kuna maambukizi na kwenye mikutano hakuna? Fauka ya haya, kwanini kuingiza nchi kwenye wimbi la kampeni za uchaguzi kana kwamba uchaguzi ndio mahitaji msingi ya raia? Chaguzi ngapi zimepita na bado hali za raia kila kukicha zinazidi kua mbaya.

Kudharau elimu ya Dini kunaingia katika ileile itikadi potofu ya Kiilmaania inayotenganisha Dini na Maisha. Itikadi hii huwapa wanadamu nafasi ya kudharau Dini na elimu yake. Jambo hili lapaswa liamshe Waislamu wafahamu kwamba serikali yoyote inayobeba ilmaaniya katu haiwezi kudhamini waalimu wa Madrasa wala elimu ya Dini yetu. Fauka ya haya, Mfumo wa Kibepari umehujumu malengo ya elimu kwa ujumla kwa kuifungamanisha na maslahi ya kiuchumi. Kwa mtazamo huu,serikali za kibepari, elimu ya dini huonekanwa kukosa manufaa yoyote yale ya kimada hivyo hubakia kudharauliwa.

Utawala wa Khilafah, utatoa elimu kwa watoto wote pasina na ubaguzi kwa lengo la kuendeleza maarifa mbali mbali kama sheria, uhandisi na matibabu. Hivyo, Khilafah itajenga majengo ya taasisi za Kielimu kuanzia chekechea hadi chuo kikuu yataimarishwa na kuwekwa maktaba na maabara ya kutosha. Mbali haya waalimu kwa ujumla watapewa heshima yao na kutunzwa maisha yao. Yote haya yatafanywa kwa lengo la kuwa na wataalamu na mujtahiduna watakaoletea raia ustawi wa kielimu na wa kimaisha jumla na kuwawezesha kuwa na ufanisi sio tu wa hapa duniani bali na kesho akhera.

**Shabani Mwalimu**

**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**

# HABARI NA MAONI

# Muislamu Anayedaiwa Kuwa 'Gaidi' Hastahili Kuachiliwa na Mahakama chini ya Tawala za Kisekula!




**Habari:**

Mnamo Jumatano, 7 Oktoba 2020 Hakimu Mkuu mjini Nairobi Francis Andayi alihukumu kuwa Liban Abdillahi Omar hana makossa katika tukio la kigaidi la Westgate. Mnamo Alhamisi, 8 Oktoba 2020 dakika chache baada ya kutoka makao makuu ya Kitengo cha Kupambana na Ugaidi (ATPU) kilichoko Upper Hill, Abdillahi Omar 'alitekwa nyara' na wanaume waliokuwa wamebeba bunduki. Tukio hilo lilitokea ilhali Omar alikuwa pamoja na dada zake ndani ya gari la teksi.

**Maoni:**

Tukio hili jipya la 'utekaji nyara' linatokea baada ya lile la mwisho lililotokea mnamo 16 Agosti 2020 ambapo Sheikh Khalid Swaleh, Ustadh Juma Shamte na Hassan wote kutoka Markaz Noor iliyoko Mtondia, Kaunti ya Kilifi. Watekaji nyara walidaiwa kuwa ni maafisa kutoka Kitengo cha Kupambana na Ugaidi (ATPU) ambao walivamia majengo hayo mwendo wa saa 7 usiku (Daily Nation, 16/08/2020). Kabla ya tukio la 16 Agosti kulikutokea shambulizi za kidhalimu mnamo Jumamosi, 30/05/2020 eneo la Kibundani Kaunti ya Kwale, ambapo Waislamu waliamkia taarifa za kuuliwa kwa Muislamu mwanamume, Mohamed Rahma Mapenzi (miaka 41), watoto wake wawili, Swalia Rahma (miaka 6) na Idd Rahma (miaka 3). Kwa kuongezea wanachama wa familia ya marehemu walijeruhiwa vibaya mno huku mkewe aliyekuwa na mimba ya miezi minane, Mwanahalima Mwachili alipoteza mimba yake wakati alipokuwa amepelekwa Hospitali ya Msambweni akiwa hali mbaya. (The Standard, 31/05/2020).

Tukio hili jipya ni thibitisho kuwa Kenya ni dola ya kimafia ya kisekula ya kidemokrasia ambayo inadai kuwa inaheshimu hukumu za kisheria ilhali kiuhalisia inakwenda mbio kukandamiza uhuru wa mahakama. Kile kinachoitwa utekaji nyara ni njama tu ya asasi za kiusalama za serikali kuzitia hofu akili na mioyo ya Waislamu. Zaidi ya hayo ni kutuma ishara kwa maafisa wa mahakama kwamba kinachotakiwa kutoka kwao kwa mujibu wa kesi zinazohusiana na 'magaidi na wenye misimamo mikali' ni kufungwa na kwamba kuachiliwa hakutakikani katika mchakato mzima!

Kenya imezama ndani mno katika kuwatoa kafara raia wake kwa jina la kupigania vita vinavyosukumwa na Wamagharibi dhidi ya Uislamu na Waislamu kwa kisingizio cha kupambana na ugaidi na misimamo mikali. Sheria na sera za Kenya zinaathiriwa na mabwana zake Wamagharibi wakiongozwa na Uingereza na washirika wake. Na ndio sababu walivamia Somalia ili kwenda kulinda maslahi ya bwana wake kwa jina la kupiga vita Alshabab, kundi ambalo vibaraka wa Wamagharibi wamepenya ndani yake na kuliongoza.

Na ndio maana lilikuwa sio jambo la kushangaza kwa

*Endelea... UK 5*



Email: info@uqab.or.ke

rais wa Kenya kuzuru Ufaransa kwa ziara ya siku tatu kuanzia 30 Septemba 2020 na kisha wakati anarudi nchini akaizuru Misri. Nchi mbili hizo zinajulikana kwa sera zao ovu dhidi ya Uislamu na Waislamu ambapo rais wa Misri anajulikana kwa kuwa dhalimu kiasi kwamba ameivunja misikiti na kupiga marufuku maandishi ya Kiislamu kwa kisingizio cha kupigia debe misimamo mikali! Kwa upande mwingine rais wa Ufaransa ana andaa uzinduzi wa sera mnamo Disemba 2020 zinazolenga kupambana na ule unaoitwa ‘Uislamu wa siasa kali’ ambao hauendani na sheria za kisekula za Jamhuri ya Ufaransa.

Ni wajibu kwa Waislamu nchini Kenya na duniani kote kufahamu uhalisia unaouzunguka Uislamu na Waislamu leo. Uhalisia ni kuwa yeyote anayebeba itikadi ya hakuna kinachostahiki kuabudiwa isipokuwa Mwenyezi Mungu na Muhammad ni Nabii Wake; na kisha akajikaza kuishi kwa mujibu wa itikadi hiyo; anazingatiwa kuwa ni adui na tawala za kisekula kwa maana ni ‘gaidi au mwenye misimamo mikali’ anayestahili kupigwa vita ili kubeba itikadi ya kisekula ili kuwa ‘Muislamu wa kati na kati’ anayepima vitendo kwa msingi wa maslahi na manufaa (sheria za kisekula)!

Uislamu na Waislamu wataendelea kutaabika chini ya tawala hizi za kisekula za kirasilimali kwa zinahofia kurudi kwa Uislamu kama mfumo mbadala katika ulingo wa kiulimwengu. Ni muhimu kutambua kwamba njia pekee ya kujinasua na ukandamizaji na mateso haya ni kuunga juhudi na kufanyakazi na Hizb ut Tahrir, chama cha Kiislamu cha kisiasa. Chama ambacho kinaongoza katika kurudisha maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha Khilafah kwa njia ya Utume. Khilafah ndio mlinzi na ngao ambayo italinda Uislamu, Waislamu na wanadamu kwa ujumla dhidi ya njama za maadui wa Uislamu na Waislamu. Ni chini ya Khilafah ambapo Waislamu watatawaliwa kwa mujibu wa Shari’ah ya Kiislamu na kuwapelekea kupata heshima na hadhi na kuhifadhi damu, mali na matukufu yao. Kwa kuongezea, wanadamu watafurahia ustawi, amani na utulivu wa kweli chini ya kiongozi muadilifu Khalifah. Mwenyezi Mungu (swt) asema:

وَعْدَ ٱللَّهِۖ لَا يُخْلِفُ ٱللَّهُ وَعْدَهُۥ وَلَـٰكِنَّ أَكْثَرَ ٱلنَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ* بِنَصْرِ ٱللَّهِۚ
يَنصُرُ مَن يَشَآءُۖ وَهُوَ ٱلْعَزِيزُ ٱلرَّحِيمُ*وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ ٱلْمُؤْمِنُونَ

“Na siku hiyo Waumini watafurahi. Kwa nusura ya Mwenyezi Mungu humnusuru amtakaye. Naye ndiye Mwenye nguvu Mwenye kurehemu. Ni ahadi ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu havunji ahadi yake. Lakini watu wengi hawajui. [Ar-Rum 30: 4 – 6].

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Enyi watu wa Kinana! Je! Hamtaivunja Serikali Hii Ambayo Imezivunja Nyumba za Mwenyezi Mungu na Nyumba Zenu?

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Sisi tunaishi katika mazingira ya kupanuliwa kwa mapinduzi ya Januari ambayo hayakuisha, kama Magharibi na wanaume wake miongoni mwa wanajeshi waliochukua madaraka baada ya mapinduzi walivyodhani, tunaona mawimbi ya mapinduzi mfululizo ambayo yanaibuka na wakati mwingine kufifia, yakizuiwa kufikia mizizi yake na kilele cha kupasuka kwake kupitia kizuizi cha hofu ambacho serikali imekiregelea kupitia mauaji ya Rabaa, al-Nahda na kwengineko na kwa ala za ukandamizaji wake ambazo daima huelekezwa kwa watu bila ya ubaguzi wakati wa makabiliano yake na watu wa Misri na dini yao juu ya haki, na kutofaulu kwa watoto wao kutoka katika jeshi kwa kutosimama na jamaa zao dhidi ya twaghut.

Serikali hii, au tuseme genge hili tawala, lilifanya kazi kuonyesha mvutano huu kuwa ni kati ya serikali na kikundi cha watu, na kuwafanya wale wote wanaopinga maamuzi yake kana kwamba ni katika kundi hilo, wakati ukweli ukiwa wao hawawakilishi dola, lakini badala yake wao waliinyakua na kuiba rasimali na neema zake na kuzipeleka Magharibi bila gharama yoyote. Na kundi hilo haliwakilishi watu wala mapinduzi, bali wao walikuwa ni sababu ya moja kwa moja ya kurudi kwa genge la jeshi katika uhai wao baada ya mapinduzi ya Januari kwa ulimbukeni wao.

Genge hili la majenerali wa Amerika linatambua kuwa halimiliki suluhisho kwa shida za watu na halijui kwamba maamuzi yake mabaya yatasababisha mlipuko, ambapo hautafaa utumiaji wa chuma na moto kukandamiza watu au kipimo cha dawa za kutuliza maumivu ambazo hutangaza kwenye vyombo vya habari ili kuwatuliza watu, wala safari ya kusafiri kati ya wanaonufaika na wadau wa maslahi ili kujaribu kuwadhibiti wanamapinduzi. Na laiti udhibiti huu ungekuwa wa kihakika kwa vitendo na zawadi zenye kushikika, bali kwa maneno matamu na matamanio yaliyotawanyika hapa na pale, kana kwamba kuna mtu anasambaza mangati kwa watu!

Wakati serikali ikiendelea kwa ukali na kiburi kilichoonyeshwa na mkuu wa genge hilo akitishia jeshi kuteremka katika kila kijiji nchini Misri kutekeleza maamuzi yake ya kubomoa nyumba na misikiti, na hakuthubutu kushambulia kanisa hata moja huku akibomoa zaidi ya misikiti sabiini kwa kisingizio kwamba iko kwenye ardhi ya serikali, hii ni baada ya miaka mingi ya misikiti kufungwa moja kwa moja baada ya kila swala na kutoruhusiwa pia ndani yake shughuli yoyote, huku makanisa yakifunguliwa kwa saa nzima na genge hili likiwa halithubutu kupunguza dori zake au kuyazuia kutangaza fikra yake. Kwa hakika, hili haliwakeri, bali Uislamu ambao unatafuta kurudisha haki za watu ambazo wanazisulubu na kuzipora, ndio unaowakera.

Kisha wanajitokeza kwetu Masheikh watiifu wa serikali, wakidai ubatilif wa swala katika misikiti hiyo, na ulazima wa kuibomoa bila ushahidi wowote na ulazima wa kuzibomoa nyumba za watu ambazo zinawasitiri na ambazo wamezijenga kwa kazi yao na jasho lao kwa miaka mingi na kuweka mali zao zote na akiba ndani yake, katika hali ya kutokuwepo kabisa kwa dola ambayo ni wajibu juu yake kuwachunga, hadi genge likaja kuzibomoa nyumba hizo juu ya vichwa vyao na kuwatupa nje wao na watoto wao, huku wakiwa wamejikunyata ...

Huku majumba, hoteli, maduka, sehemu za biashara na maeneo mengine yakiwa yamejengwa kwa ajili ya wanachama wa genge hili na wale waliokusanyika kwenye ardhi hiyo inayomilikiwa na serikali, kama wanavyodai, na hakuna mtu aliyesubutu kuyagusa, achilia mbali kuyabomoa, na huku serikali ikiweka hali ya ukali kwa watu wote

***Endelea... UK 7***

isipokuwa wanajeshi, ambao huwaongeza mishahara yao na pensheni mara nyingi, mbali na kuwapa fadhila ya kufurahia huduma ambazo watu wengine hawazifurahii, labda wao ni jamii nyingine isiyokuwa ya kibinadamu, na pengine kwa hili ndio maana wanashiriki katika kuua watu!

Na mbele ya ubomoaji wa nyumba na misikiti juu ya vichwa vya watu, walitoka nje na kusema haki na kweli (hakuna Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Mwenyezi Mungu na al-Sisi ni adui wa Mwenyezi Mungu), hata ikiwa yeye sio adui pekee, bali genge lote la majenerali na wale wanaowasaidia wote ni maadui wa Mwenyezi Mungu, Mtume Wake, dini yake na Ummah wake.

Enyi watu wa Kinana! Hakika katika jukumu la dola kwa raia wake ni kushibisha mahitaji ya kila mmoja wa raia wake kwa kiwango cha kutosha katika vitu tatu: chakula, mavazi na makazi, na kumpa mahitaji ya ziada kadri inavyowezekana, na katika hili hakuna tofauti kati ya Muislamu na asiyekuwa Mwislamu, badala yake kila mtu ni sawa, na lazima iidhamini jamii kwa ujumla wake vitu vitatu kwa kiwango cha juu kabisa na ikiwezekana bila malipo: usalama, elimu na huduma za afya, kwa usalama inamaanisha kusalimika maisha yao, pesa na akiba, na kuhifadhi dini yao na utu wao, sio kubomoa nyumba zao, kukiuka utu wao na kuwaibia akiba yao kama genge hili linavyofanya sasa. Kwa katika elimu, ni kudhamana kiwango cha juu kabisa cha elimu ikiwezekana bila malipo kwa wote. Hakuna tofauti kati ya Muislamu na asiyekuwa Muislamu, wala matajiri na maskini, wala hakuna shule za matajiri na zingine kwa masikini. Badala yake, dola inaondoa utabaka na uaswabiya na kila kitu kinachozalisha haya. Ama katika usimamizi wa afya, itatoa madaktari na madawa kwa watu wote kwa kiwango cha juu kabisa na ikiwezekana bila malipo. Hakuna tofauti baina ya tajiri na masikini wala Muislamu na asiyekuwa Muislamu, bali kwa watu wote kwa usawa. Inajishughulisha yenyewe na inafanya muamala yenyewe, hakuna muamala spesheli kwa wasomi, majenerali, wala utofauti kwa wanajeshi au wengine, bali kila mtu ni sawa.

Lakini, haya yote hayatimizwi kwa ahadi za genge la majenerali, wala hayamilikiwi na urasilimali ambao wanatawala kwao. Badala yake, yanamilikiwa na Uislamu, ambao wanaupiga vita na mfumo wake, ambao wanatafuta kuuzuia katika kurudi kutawala ndani ya dola ya Khilafah Rashida kwa njia ya Utume.

Enyi watu wa Kinana! Yeyote anayevunja nyumba za Mwenyezi Mungu na nyumba zenu hastahili kuwatawala, na kumuasi kwenu ni wajibu, na hakika mapinduzi yenu hayakamiliki na kamwe hayatakamilika isipokuwa kwa kuubeba Uislamu na mradi wake wa kihadhara ambao unahakikisha utu wenu, uhuru wenu na ustawi wenu, na unakuhakikishieni uadilifu kama uadilifu wa Umar ambao mnaujua. Basi msikubali chochote kisichokuwa Uislamu na mfumo wake na dola yake Khilafah Rashida kwa njia ya Utume, dola kamili inayotabikisha Uislamu kwa ukamilifu wake na kwa uadilifu wake. Hii ni haki yenu basi idaini wala msikubali chochote chini yake ili msirudi kwenye nukta ile ile na kutawaliwa na genge lile lile kwa majina tofauti!

Enyi wenye ikhlasi katika jeshi la Kinana! Basi na upooze kila mkono ulioshiriki katika kubomoa misikiti na nyumba za wanyonge miongoni mwa watu na wasio na usaidizi, Mwenyezi Mungu (swt) asema:

**وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن مَّنَعَ مَسَاجِدَ اللهِ أَن يُذْكَرَ فِيهَا اسْمُهُ وَسَعَى فِي خَرَابِهَا أُوْلَـئِكَ مَا كَانَ لَهُمْ أَن يَدْخُلُوهَا إِلاَّ خَآئِفِينَ لهُمْ فِي الدُّنْيَا خِزْيٌ وَلَهُمْ فِي الآخِرَةِ عَذَابٌ عَظِيمٌ**

“Na ni nani dhaalimu mkubwa kuliko yule anaye zuia misikiti ya Mwenyezi Mungu kutajwa ndani yake jina lake na akajitahidi kuiharibu? Watu hao haitawafalia kuingia humo ila nao wanaogopa. Duniani watapata hizaya na Akhera watapata adhabu kubwa.” [Al-Baqara: 114] kwani ni nani aliye na dhalimu zaidi kuliko serikali hii unayovunja nyumba za Mungu?! Serikali hii ambayo mnaihami ndiyo ambayo ni wajibu ivunjwe, sio misikiti na nyumba za watu ambazo zimebomolewa chini ya masikio, macho, na uchungaji wenu, bali kwa mikono yenu wenyewe, mtakutana vipi na Mola wenu kwa mikono iliyochafuliwa na damu ya watu wasio na hatia na kwa nyuso ambazo hazikugubikwa kwa vumbi la Jihad katika Njia ya Mwenyezi Mungu, bali zimegubikwa vumbi la vifusi vya misikiti na nyumba za watu?!

Basi andaeni jibu lenu na hoja yenu, au tangazeni kuwa mbali na genge hili la maafisa wa jeshi la Amerika na liacheni lizame bila yenu, kwa sababu Amerika haitajilinda na watu hawataionea huruma, kwa hivyo msiwe katika kundi lake, na mjue kuwa yote ambayo serikali hii unakupeni ili kuhakikisha uaminifu wenu ni kiasi kidogo cha baadhi ya haki zenu, kwa hivyo msizichukue kama hongo na kisha mkawapa watoto wenu pesa chafu (Al-Suht), na chukueni haki zenu kamili kwa kuwapendelea jamaa zenu katika mapinduzi yao na mnusuru mradi pekee wa Ummah wa kihadhara ambao Hizb ut-Tahrir unauwasilisha na ni dhamana ya

***Endelea... UK 8***

haki, uhuru na utu wa watu kwa kutabikisha Uislamu kikamilifu na kwa upana katika dola yake ya Khilafah Rashida kwa njia ya Utume, huenda Mwenyezi Mungu akawasamehe yale yaliyotangulia na akakubali kutoka kwenu na akafungua mikononi mwenu na Misri ikaokoka na hata Ummah mzima kupitia nyinyi. Je! Mtakuwa na furaha iliyoje lau mtafanya hivi, na Misri itakuwa na utukufu ulioje, na Uislamu na Waislamu, kupitia nyinyi, na mtayakumbuka haya tuyokuambieni sasa na tunalikabidhi jambo letu kwa Mwenyezi Mungu.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُواْ اسْتَجِيبُواْ لِلّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا دَعَاكُم لِمَا يُحْيِيكُمْ وَاعْلَمُواْ أَنَّ اللّهَ يَحُولُ بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ

Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa. [Al-Anfal: 24]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Misri**

# Ufupisho wa Hotuba Ovu ya Macron dhidi ya Uislamu na Waislamu



Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron mnamo Ijumaa, 2 Oktoba 2020 katika Kasri la Elysee alitoa hotuba ya kihistoria na yenye chuki dhidi ya Uislamu na Waislamu. Hotuba hiyo ilipeperushwa ulimwenguni kote. Hotuba hiyo ilikuwa inafuatia ziara ya Macron nchini Lebanon mnamo Jumanne, 1 Septemba 2020; ambapo alizungumza kuhusu kwa nini hakulikashifu jarida la vichekesho la Charlie Hebdo kwa kuchapisha tena vibonzo vya kukufuru dhidi ya Mtume wetu Muhammad (saw). Alisema, "Sio nafasi ya rais wa Jamhuri kutoa hukumu juu ya maamuzi ya mwandishi wa habari au idhaa ya habari, la. Kwa sababu tuna uhuru wa vyombo vya habari." (Reuters, 15/09/2020).

Hotuba hiyo iliangazia tishio la unaoitwa Uislamu wa kujitenga. Ilisisitiza mwito kwa taifa kujikusanya na kuchangamkia uamsho unaolenga kulinda maadili na misingi ya jamhuri ya kisekula ya Kifaransa ambayo yanashambuliwa na Uislamu mkali. Kwa kuongezea aliliomba taifa kumuunga mkono yeye na Serikali yake katika mchakato wa kuja na mswada mkali ambao utapelekwa katika Baraza la Mawaziri mnamo Ijumatano, 9 Disemba 2020 na Waziri na Naibu Waziri wa Ndani ili upitishwe kabla kupelekwa Bungeni kwa mjadala na kupitishwa kuwa sheria. Mswada huo unatajwa kuwa ni uboreshaji wa sheria ya mwaka 1905 na inalenga kuuboresha usekula na kuyajumuisha maadili ya jamhuri.

Sheria hiyo itakuwa ndio marudio ya kimkakati yatakayojumuisha nguzo tano muhimu zifuatazo:

**Kwanza,** kuweka hatua ambazo zitapigia debe kutoegemea mrengo fulani katika nyanja ya utulivu wa umma na huduma za umma. Hatua hizo zinalenga kutatua sintofahamu zinazoshuhudiwa aghalabu na wale wanaotaka na wanaotoa huduma za umma kama vile huduma za kuogelea na mabasi. Kwa mfano, baadhi ya Waislamu wanadaiwa kutaka wapewe huduma kwa upendeleo kwa kudai wanawake na wanaume watenganishwe na watengewe muda tofauti katika sehemu za kuogelea. Kwa upande mwingine, wengine wanafanyiwa ubaguzi kutokana na mavazi yao na hivyo

*Endelea... UK 9*

kunyimwa nafasi katika huduma za usafiri. Hivyo basi, hatua hizo zitalenga kuzisawazisha jinsia zote pasina kuzingatia dini zao kwa kuwa Ufaransa ni jamhuri ya kisekula.

**Pili,** kuboresha udhibiti wa miungano ndani ya ardhi ya Ufaransa na kuhakikisha kuwa ipo kwa ajili ya kuhudumikia na kupigia debe misingi ya jamhuri ya kisekula ya Kifaransa. Kwa kuongezea, ili kuziwezesha asasi za Dola katika kutia saini na miungano na kuipa misaada ya kifedha kwa sharti kwamba haikiuki maadili ya jamhuri ya kisekula ya Kifaransa. Lau itakwenda kinyume na makubaliano ya mkataba, basi irudishe pesa na itakabiliwa na kuvunjwa.

**Tatu,** ili kuziboresha sheria za mwaka 1882 na 1969. Kiudhati ni shule ndani ya Jamhuri ndio chungu cha kuyeyusha. Zaidi ya hayo, shule ndiyo inayoasisi usekula na kuhifadhi maadili ya jamhuri ndani ya mioyo na akili za wanafunzi. Watoto wanalindwa dhidi ya ushawishi wa dini kupitia kwenda shule. Hivyo basi, kuanzia mwanzo wa kalenda ya masomo ya 2021, kila mmoja kuanzia miaka 3 lazima aende shule na kusoma nyumbani hakutoruhusiwa isipokuwa kwa udhibiti mkali tena kwa sababu za kiafya. Nidhamu ya elimu itakuwa moja pekee na ni ile ya EILE na ambayo itakuwa chini ya udhibiti mkali wa Waziri wa Elimu ya Kitaifa nchini Ufaransa. Masomo ya kufundishwa lazima yakuze mapenzi kwa jamhuri ya kisekula na kupigia debe hisia za uhuru. Shule zote lazima zijifunge na maelekezo ya maadili ya jamhuri ya kisekula ya Kifaransa na lau zitakiuka zitafungwa.

Nne, kujenga Uislamu unaooana na maadili na misingi ya kijamhuri ya kisekula ya Kifaransa. Ili kuwa na Uislamu wa Kifaransa, Waziri wa Ndani atafanyakazi na Baraza la Ibada la Waislamu nchini Ufaransa ili kupambana na ushawishi kutoka ng'ambo. Jamhuri ya Ufaransa imeamua kusitisha kwa amani kuwafunza na kuwaleta maimamu kutoka Uturuki, Moroko na Algeria ndani ya ardhi ya Ufaransa. Kutakuwepo na udhibiti na utekelezaji mkali wa sheria ya mwaka 1905 kuhusiana na udhamini wa kifedha kutoka ng'ambo kwa misikiti. Baraza la Ibada la Waislamu nchini Ufaransa litaweka mpango wa kuwafunza na kuwapigia debe maimamu na wasomi ambao watautetea Uislamu unaooana na maadili ya kisekula ya Kifaransa. Baraza la Ibada la Waislamu nchini Ufaransa litaorodhesha kozi za mafunzo, litatoa vyeti kwa maimamu, litaandaa mkataba ambao maimamu wakiukiuka watafutiliwa mbali na watapangilia namna ya utekelezaji wa safari ya hajj kwa ajili udhamini wa dharura wa kifedha kutoka kwa jamhuri ya Kifaransa. Hatimaye, Jamhuri itatoa msaada kwa miradi iliyoanzishwa na Waqf wa Uislamu nchini Ufaransa wa kitita cha uro milioni 10 katika nyanja za thaqafa, historia na sayansi.

**Tano,** ili kuangazia uwezo na ushindi wa Jamhuri dhidi ya Uislamu pale ilipoiangamiza Dola ya Kiislamu ya Khilafah mnamo 3 Machi 1924 na kusimamisha juu ya ardhi yake ambayo ilikuwa imeungana lakini Jamhuri na washirika wake wakaigawanya kuwa vijidola 54 na kuweka juu yake nidhamu ya kijamhuri iliyopo mpaka leo. Hivyo basi, ahadi ya Jamhuri lazima ihuishwe kwa kuzitekeleza sheria zake kwa ukali na hatimaye mapenzi na mustakbali wa Jamhuri utashinda.

Kwa kutamatisha, ufupisho huo hapo juu unafichua wazi kufeli kamili kwa mfumo wa kirasilimali wa kisekula na nidhamu zake zenye sumu katika kutoa usalama na ustawi wa kweli kwa wanadamu. Majanga yao na kufeli kwao kunashuhudiwa duniani kote na kuzidishwa na janga linaloendelea la Covi-19 ambalo limesambaratisha hadhara ya Kimagharibi ambayo inanawiri kwa msingi wa ubaguzi wa rangi na pengo la tajiri na masikini. Kwa upande mwingine, Uislamu unachomoza duniani kote na muda wowote kuanzia sasa utakuwa ndio nguvu kuu ya kisiasa katika ulingo wa dunia. Kwa hiyo hizo patashika mpya kutoka kwa jamhuri ya Kifaransa, mlinzi wa makubaliano ya Sykes-Picot ambayo ndio chanzo cha mauaji na uporaji usioingia akili wa rasilimali za Mashariki ya Kati hadi Afrika. Uongozi wa Kifaransa unajulikana daima kwa namna unavyo kwenda mbio kujipa sura mpya kila unapokabiliwa na majanga ili kuwahadaa watu kuwa upo imara lakini kiuhalisia unatapatapa kubakia usije ukatumbukia. Hatimaye, Macron anadanganya alipotangaza kwamba Uislamu upo katika janga, ilhali uhalisia unaonyesha kinyume. Ukweli ni kwamba mfumo wa kirasilimali wa kisekula upo katika chumba cha mahututi unasubiri kutangazwa kifo chake kwa kuwasili kwa Khilafah iliyosimama kwa njia ya Utume. Kwa kuwa Uislamu ndio njia pekee mbadala yenye uwezo na iliyowahi kujaribiwa kutatua matatizo ya wanadamu wote pasina kuzingatia rangi, dini au vyeo vyao. Kwa hiyo uongozi wa Kifaransa umejitwika kampeni na njama ovu ambazo daima zimefeli kwa misingi ya kirongo kwamba Uislamu ni mkali na Waislamu ni watu wenye misimamo mikali ili kuweza kuwakatisha watu tamaa ili wasiukumbatie! Sasa ndio wakati wa #KurudishaKhilafah.

قَدْ بَدَتِ ٱلْبَغْضَآءُ مِنْ أَفْوَٰهِهِمْ وَمَا تُخْفِى صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ


"Imekwisha fichuka chuki yao katika midomo yao. Na yanayo ficha vifua vyao ni makubwa zaidi." (Aal-e-Imran: 3: 118).


**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Kuanguka kwa Dini Katika Mfumo wa Kisekula sio Ajabu, ni Jambo Lakutarajiwa

**Fatima Musab**
**Mwanachama wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

Utafiti wa karibuni umeonyesha kuwa kuna muanguko wa dini kiulimwengu. Ikiangaliwa katika jamii za Kimagharibi, na kukua kwa uliberali wa kisekula, hili halishangazi. Kwa mujibu wa makala katika Wizara za Mambo ya Nje, kuna idadi inayoongezeka ya watu ambao “hawaoni dini kuwa ni chanzo muhimu cha usaidizi na cha maana katika maisha yao.” Wao “wamekuwa ni watu wasioibeba sana dini kwa sehemu fulani kwa sababu hawaihitajii tena katika kuzingatia aina za maadili ya kijinsia na ya kingono ambapo dini kubwa ulimwenguni zimekuwa zikisisitiza kwa karne nyingi.” Makala ya Wizara za Mambo ya Nje imelenga juu ya kuanguka kwa dini katika Ulaya na Asia. Lakini kwa mujibu wa BBC, muanguko huu pia unaonekana katika Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini ambako kuna ongezeko la idadi ya watu wasioshikamana dini sana.




Source: BBC

**Je, muanguko huu unapaswa kutushangaza?**

Hapana, muanguko huu katika dini haukuja kama mshangao. Msingi hasa wa usekula wa kiliberali ni kuwa dini imejifunga na ibada ya kibinafsi na kwa hivyo, haina jukumu katika kupanga na kutawala masuala ya kijamii. Dini inaonekana kuwa ni suala la imani ya kibinafsi ambayo hutekelezwa kibinafsi. Kwa hiyo, tunaishi katika dunia ambayo usekula unaongezeka na kutoa “kipaumbele kikubwa kinachoongezeka cha kujieleza na chaguo huru, pamoja na msisitizo unaoongezeka juu ya haki za binaadamu, uvumilivu kwa walio nje, uhifadhi wa mazingira, usawa wa kijinsia na uhuru wa kusema.” (Chanzo: Wizara ya Mambo ya Nje)

Tatizo ni hili; kama tunaitenga dini na maisha ya kibinafsi, basi vipi tutachora mstari? Je, tutaruhusu dini kufundishwa katika mfumo wetu wa elimu? Tutaruhusu dini kuongoza matendo yetu wakati tunashughulika na marafiki zetu na familia, au ni kuiruhusu dini kuelekea zaidi katika kuifunga kwenye maisha yetu ya kibinafsi. Kama tunaruhusu dini kuongoza maisha yetu hapa, itakwenda kwa umbali gani? Je, itumike kama msingi wa maamuzi yetu wakati tunapokabiliana na sintofahamu? Itakuwaje kama sintofahamu hii ni katika masuala ya kisheria?

Ukweli ni huu – kuanguka kwa dini katika jamii inayoelekea zaidi kwenye uliberali isitushangaze. Wanayo jamii ambayo wazo la kuwa na dini sio msingi wa fikra na matendo, bali uliberali ndio msingi. Matokeo yake, dini sio sehemu ya maisha ya watu. Manufaa ya kiuchumi ni nukta inayolengwa katika kufanya maamuzi. Maadili ni suala linaloweza kujadiliwa kulingana na manufaa na ubinafsi. Na dini hutumika kama ni chombo cha wanasiasa; ili kudumisha uungaji mkono wa mfumo wa kiliberali katika nchi ambazo awali zilishikamana sana na dini, kuhakikisha mshikamano wa kijamii kwa kuwa ubinafsi katika uliberali huvunja fungamano la kijamii na kueneza fikra kama ‘maisha ni kwa wenye kustahiki’.

*Endelea... UK 11*

Usekula huu haukupelekea kwenye jamii ilio imara. Ni kinyume kabisa, umetengeneza na kuongeza matatizo ya aina mbali mbali bila ya utatuzi wowote. Ubaguzi wa rangi, taasubi ya kijinsia, uchukivu kwa wanaovunja maadili, unyanyasaji wa kijinsia, vurugu za utumiaji wa silaha, mauaji, mateso, mauwaji ya halaiki; hii ni mifano michache tu ya matatizo ambayo jamii ya kiliberali imeshindwa kuyatatua.

Takwimu kuhusiana na kuanguka kwa dini zisitufadhaishe, zitufanye tufikiri. Ongezeko la kutoridhika kwa jamii ya Wamagharibi na athari ya COVID, imetufanya tuwe kwenye hatua ya mabadiliko katika historia. Mfumo wa Kimagharibi umejaa nyufa na nyufa hizo zinaongezeka na kuwa wazi zaidi. Wanatafuta njia ya kuziba nyufa hizo, au kugeuza mazingatio yetu kwa kueneza hisia zinazopingana na dini, hisia zinazopingana na uhamiaji. Ni mbinu ambayo daima wamekuwa wakiitumia wanapokuwa na matatizo – tengeneza adui ili Ummah wa Kiislamu pamoja na watu wao wenyewe wasitafute badali na kutafuta masuluhisho ya matatizo yao katika Uislamu. Lakini hii itukumbushe sisi kwa nini tunahitaji kufanya kazi ya kusimamisha Dola ya Kiislamu na kutazama uhalisia wa leo kama fursa.

Tunahitaji kukumbuka kuwa Uislamu sio kama dini nyengine – inakusanya fikra na masuluhisho ya matatizo ya wanaadamu kwa kina na kuathiri kila kipengele cha maisha yetu. Historia ya Uislamu na mafanikio ya Dola ya Kiislamu ni ushuhuda kwa hili. Hali ya sasa ya mambo na kuanguka kwa dini ni jambo likutarajiwa kwa sababu Uislamu hautekelezwi kwa ukamilifu wake.


**Tunahitaji kusimamisha tena Dola ya Kiislamu**

Kwa kweli hatuwezi kuitenganisha dini na dola – tunahitaji msingi wa kuongoza matendo yetu na kama uhalisia wa sasa unavyoonyesha, akili zetu wanaadamu zikiwa na haja na matashi, sio msingi wa kuhukumu kilicho kizuri na kibaya. Kwa hivyo, dini sio kitu ambacho kinaweza kutengwa katika maisha yetu ya kibinafsi, kuna matatizo mengi sana na mivutano ambayo inayowasili. Dini haiwezi kufungwa na kipengele kimoja cha maisha yetu. Hilo halitakuwa tatizo la Uislamu – pindi utapotekelezwa kama inavyopasa, kwa usimamishaji tena wa Dola ya Kiislamu.

(الْيَوْمَ أَكْمَلْتُ لَكُمْ دِينَكُمْ وَأَتْمَمْتُ عَلَيْكُمْ نِعْمَتِي وَرَضِيتُ لَكُمُ الْإِسْلَامَ دِينًا)

”Leo nimekukamilishieni Dini yenu na nimekutimizieni neema yangu, na nimekupendeleeni Uislamu uwe ndio Dini” [Al-Maida: 3]

Pia ni muhimu kukumbuka kuwa wakati mfumo wa Kimagharibi na wafuasi wao wamejaribu kutusukuma kuubeba uliberali, Ummah wa Kiislamu umedumisha mshikamano wao kwa Uislamu.




Source: PewResearch

Lakini ni lazima tusisahau kuwa Uislamu hautekelezwi kama inavyotakiwa. Kuisimamisha Dola ya Kiislamu humaanisha kukubali kuwa Sheria za Mwenyezi Mungu ndio msingi wa maamuzi yetu yote. Hatuwezi kuwa na mfumo wa kisekula, na baadaye kutarajia Uislamu uafikiane nao. Chini ya Uislamu, maadili sio kitu cha kujadiliwa. Mwenyezi Mungu, Muumba wetu, ambaye anatuelewa sisi zaidi ametupatia sheria juu ya namna ya kuamiliana baina yetu.

Masuala ya dini na dola lazima yaunganishwe na kuenezwa kwenye kila kipengele cha maisha yetu, na kuathiri jamii na mtu binafsi. Sheria ambazo zinatuongoza, katika kila kipengele cha maisha yetu, na kuwaongoza watawala wetu kuhakikisha kuwa watu wanalindwa na kupewa haki zao.

# JIBU LA SWALI

# Mzozo Kati ya Uturuki na Ugiriki katika Eneo la Mashariki mwa Mediterranea




**Swali:**

Mnamo tarehe 8/10/2020, Waziri wa Mambo ya nje wa Uturuki Mevlut Cavusoglu alifichua kwamba alikuwa amefikia makubaliano mapya kati ya nchi yake na Ugiriki. Waziri huyu alisema katika taarifa zake, kulingana na wavuti wa Turkey Now: ["Kwamba alikubaliana na mwenzake wa Uigiriki Nikos Dendias kufanya mazungumzo ya utafiti kati ya nchi hizo mbili. Hii ilikuja katika taarifa kufuatia mkutano wake na Dendias juu ya kadhia za pembeni za ushiriki wake katika Kikao cha Usalama cha Kiulimwenguni cha Bratislava nchini Slovakia. Alielezea kuwa Uturuki itakuwa mwenyeji wa mazungumzo hayo, huku Ugiriki ikiwasilisha mapendekezo ya makataa yake." (Wavuti wa Turkey Now, 8/10/2020)]. Hapo awali, Uturuki ilikuwa imezorotesha sana uhusiano wake na Ugiriki na kupambana nayo kupitia kutuma meli za utafiti za Uturuki pamoja na manuari za kusindikiza ... Je! Uhalisia wa mgogoro huu kati ya Uturuki na Ugiriki ni upi? Je! Ni upi uhalisia wa misimamo ya kimataifa juu ya mgogoro huu? Je! Amerika iko nyuma yake au Uturuki inafanya kazi peke yake? Na ni yapi maelezo ya taharuki kubwa iliyokuwa mwanzoni na kumalizika kwa makubaliano ya mazungumzo hayo? Asante.

**Jibu:**

Mgogoro wa Uturuki na Ugiriki lazima uangaliwe kwa upande wa sababu zake na athari za ndani nchini Uturuki, na vile vile vipimo vyake vya kiuchumi na kimataifa ... ili kujua, mambo yafuatayo yanapaswa kuhakikiwa, kuanzia kwa Mkataba wa Lausanne katika robo ya kwanza ya karne iliyopita:

**Kwanza: Mkataba wa Lausanne:**

1- Uturuki ina pwani ndefu zaidi kwenye Bahari ya Aegean na Mediterania ya Mashariki, lakini Mkataba wa Lausanne uliotiwa sainiwa tarehe 24/7/1923 na wawakilishi wa mhalifu wa zama hizo, Mustafa Kemal, kwa niaba ya serikali ya Bunge Kuu la Kitaifa la Uturuki jijini Ankara lililojitenga kutoka kwa Khilafah jijini Istanbul, ndio ulioifunga Uturuki na Bahari ya Aegean, ikiwa vigumu kuondoka kutoka katika pwani zake, kwani visiwa vilivyo ndani ya Bahari ya Aegean ima vyote au vingi vimekuwa mali ya Ugiriki! Hapo ndipo Mustafa Kemal alipowatuma wawakilishi wake hadi Lausanne nchini Uswizi, akipendekeza kwa Washirika kwamba serikali yake jijini Ankara, iliyokuwa imejitenga na Khilafah jijini Istanbul, inaweza kutia saini nao, washirika, mkataba ambao waliutaka! Kwa hivyo, Mkataba wa Lausanne

*Endelea... UK 13*



Email: info@uqab.or.ke

ulitiwa saini na Uswisi kati ya wawakilishi wa Uingereza, Ufaransa na nchi zingine na wawakilishi wa Mustafa Kemal, walioongozwa na Ismet Inönü kwa niaba ya serikali ya Bunge Kuu la Kitaifa jijini Ankara ...

2- Masuala ya kushtua yaliyofafanuliwa kwa kina katika mkataba huo yaliafikiwa na Mustafa Kemal na wawakilishi wake, pamoja na kile kilichokuja katika Kifungu cha 12, ambapo visiwa vyote au vingi vya Aegean vilikuwa mali ya Ugiriki, ingawa baadhi yake viko umbali wa kilomita 600 kutoka kwa bara ya Ugiriki, huku vikikutana na bara la Uturuki kwa umbali wa kilomita mbili wakati mwingine, kama ilivyo hali ya kisiwa cha Meis, ambacho ni cha Ugiriki ambacho wanakiita Kastellorizo, mbali na mji wa Kaş katika jimbo la Antalya. Ni mkataba huu ndio unaoipa Ugiriki (uhalali) kuitaka Uturuki isichimbe pwani za Uturuki kwa sababu ni haki ya kipekee ya Ugiriki chini ya Mkataba wa Lausanne! Na Ibara ya 15 inasema kwamba Uturuki inapaswa kuachilia, kwa manufaa ya Italia, haki zote na umiliki juu ya visiwa vifuatavyo: Stampalia (Astypalaia), Rhodes (Rhodes), Halki (Kharke) ... nk, na pia Kifungu cha 20: kwamba Uturuki inatambua kuunganishwa kwa Cyprus na serikali ya Uingereza kulikotangazwa na Uingereza mnamo Novemba 1914. Pia, yale yalitajwa katika kifungu cha 23 ambacho kinasema kuwa Pande (Kuu) za Mkataba zimekubali kutambua na kutangaza kanuni ya uhuru wa kupita na kusafiri, kwa bahari na anga, wakati wa amani na wakati wa vita, huko Dardanelles, Bahari ya Marmara na Bosporus! Kwa hivyo, Uturuki imepoteza, huku ikiwa na pwani ndefu zaidi mashariki mwa Mediterania, uhuru wa kusafiri ndani ya visiwa hivi katika bahari hizi, ambapo Erdogan anaikumbuka leo kama "Nchi yake ya Samawati iliyoibiwa"!

Analalamika kuhusiana nayo wakati picha ya mhalifu wa zama hizo Mustafa Kemal inaning'inia juu ya kichwa chake, ambaye ndiye aliyeidhinisha makubaliano haya huko Lausanne. Licha ya yote haya na kwamba hasubutu kumtaja Mustafa kwa neno la matusi!! Badala yake, yeye hucheza na hamasa za watu wa Uturuki kupitia kuzipa meli za utafiti majina ya viongozi wakuu wa Kiuthmani, Muhammad Al-Fatih na al-Qanuni, licha ya kuwa mbali kwake na viongozi hawa wakuu katika sera zake zote! Anatangaza, "Kila mtu anatambua kwamba Uturuki ina uwezo wa kisiasa, kiuchumi na kijeshi" kuzipasua nyaraka na ramani zisizo za haki zilizotokana na uovu na ugomvi dhidi yake." Aliongeza, "kwamba nchi yake iko tayari kufafanua jambo hili kwa kupitia uzoefu mchungu, iwe kwenye meza ya mazungumzo au katika uwanja." Al Jazeera, 5/9/2020), lakini anakomea hapa na kudhani kuwa amefanya vyema! Labda watu wa Uturuki waliona kwamba Ugiriki, ambayo haina jeshi lenye ushawishi vilivyo, ilituma wanajeshi wake kwenye kisiwa cha Meis, wakibainisha kuwa Mkataba wa Lausanne unaelezea kuondolewa kwa nguvu za kijeshi huko, na bado hawakuikabili Ugiriki kwa nguvu inayostahili!

3- Ingawa Mkataba huu ulikuwa mkataba wa hila ambao Mustafa Kemal aliukamilisha na washirika, lakini aliukamilisha kwa jina la serikali ya Bunge Kuu la Kitaifa jijini Ankara. Uingereza haikuridhika na hilo, lakini ilimtaka amalize masharti aliyowekewa, haswa kuivunja Khilafah kabisa na kuasisiwa kwa dola ya kisekula. Mustafa Kemal alitii, hii ilifanyika asubuhi ya 3 Machi 1924, wakati Khilafah ilipotangazwa kuvunjwa na dini kutengwa na serikali. Usiku huo huo, Mustafa Kemal alituma agizo kwa gavana wa Istanbul akisema kwamba Khalifa Abdul-Majid aondoke Uturuki kabla ya alfajiri ya siku iliyofuata, kwa hivyo akaenda na kikosi cha polisi na jeshi hadi katika kasri la Khalifa katikati ya usiku, na huko alimlazimisha Khalifa kupanda gari lililombeba kuvuka mpaka kuelekea Uswizi. Baada ya siku mbili, Mustafa Kemal alikusanya wana wa kiume na wa kike wa kifalme na kuwafurusha nje ya nchi. Nafasi zote za kidini zilifutiliwa mbali, wakfu za Waislamu zikawa mali ya dola, shule za kidini zilibadilishwa kuwa shule za serikali, na zikawa chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu.

Kwa hili, Mustafa Kemal alitimiza masharti manne ambayo Curzon aliyataka kutoka kwake, ambayo ni: kuivunja Khilafah kabisa, kufukuzwa kwa khalifa nje ya mipaka, kunyang'anywa fedha zake, na tangazo la usekula wa dola. Kwa hivyo, Mkataba wa Lausanne ambao ulikamilishwa kabla ya kuvunjwa kwa Khilafah ulithibitishwa na kutekelezwa baada ya kuvunjwa kwa Khilafah! Kwa hivyo, Mkataba wa Lausanne ulimalizika kwa kuvunjwa kwa dola ya Khilafah; dola ziliutambua uhuru wa Uturuki, na Waingereza waliondoka Istanbul. Matokeo yake, mmoja wa wabunge wa Uingereza alimpinga Curzon katika Bunge la House of Commons kwa kutambua kwake uhuru wa Uturuki. Curzon alimjibu akisema: "Hali sasa ni kwamba Uturuki imekufa na haitafufuka tena, kwa sababu tumeangamiza nguvu yake ya kimaadili, Khilafah na Uislamu." Kwa hivyo, Waingereza waliiondoa Khilafah na Uislamu kupitia Mustafa Kemal, licha ya upinzani wa Waislamu kote ulimwenguni kwa jumla, na licha ya upinzani wa Waislamu nchini Uturuki haswa. Kwa hivyo, hukmu kwa yale yote yaliyoteremshwa na Mwenyezi Mungu (swt) iliondolewa kutoka sehemu zote za ardhi, na hukmu kwa yasiyokuwa yale yaliyoteremshwa na Mwenyezi Mungu (swt), hukmu ya kikafiri ikabakia, na hukmu ya Taghut (ukafiri) peke yake ilibakia, ambayo inawadhibiti watu wote, na inatekelezwa kote ulimwenguni!

**Pili:** Mkataba huu uliotiwa saini na wawakilishi wa Mustafa Kemal katika jiji la Uswizi la Lausanne, ambapo Uturuki ilizuiliwa kutokana na Bahari ya Aegean, visiwa vyake na fukwe zilipewa Ugiriki, na Uturuki ilizuiwa kuichimba! Hali hii ambayo Uturuki ilikabiliwa nayo iliendelea kwa karibu miaka mia moja, kwa hivyo ni nini kilichoihamisha Uturuki sasa? Yule anayefuatilia mwenendo wa mambo atagundua kuwa kuna sababu mbili nyuma ya mgogoro huu: Kindani kwa sababu ya hali za uchumi wa Uturuki, na kinje, kwamba Amerika inasimama nyuma yake:

*Endelea... UK 14*



Email: info@uqab.or.ke

**1- Sababu za Ndani:**

a- Uturuki ni nchi inayotumia nishati na isiyozalisha, na hivi karibuni uzalishaji wake wa mafuta umefikia mapipa elfu 53 kwa siku (Shirika la Anadolu, 25/7/2020), ambayo ni idadi ndogo sana ikilinganishwa na matumizi ya mapipa milioni moja ya mafuta kila siku (Al-Araby Al-Jadeed, 22/4/2020). Inazalisha takriban mita za ujazo milioni 475 za gesi na kuagiza zaidi ya mita za ujazo bilioni 45 (Al-Jazeera Net, 31/8/2020). Kwa hivyo, Uturuki inakabiliwa na bili kubwa ya mafuta na gesi inayoingiza, ambayo ilifikia dolari bilioni 41 mnamo 2019, chini kutoka bilioni 43 kwa mwaka 2018 kwa sababu ya bei ya chini ya nishati ulimwenguni (Jarida la Uturuki la Sabah Daily, 27/2 / 2020). Hii ni sababu ambayo inaathiri sana uchumi wa Uturuki.

b- Na kwa sababu Uturuki iko kati ya nchi zinazozalisha mafuta katika eneo la Kiarabu, Iran na Azerbaijan, na kati ya nchi zinazotumia mafuta, ambazo ni nchi za Ulaya, imejenga mikakati yake mingi ya nishati kwa msingi wa kuwa "nchi ya ukanda", na bandari ya Ceyhan ya Uturuki imekuwa bandari ya kusafirisha mafuta ya Azerbaijan na mtandao wa mabomba umeanzishwa ndani yake na kupitia bandari hiyo. Sio ya mwisho ambayo ni bomba kubwa la Uturuki kusafirisha gesi ya Urusi kwenda magharibi mwa Uturuki na kutoka huko kwenda Ulaya, ambalo lilizinduliwa mnamo 8/1/2020. Licha ya ada ambayo Uturuki inakusanya kama ukanda wa nishati, bili ya mafuta na gesi bado ingali ghali sana kwa uchumi wake.

c- Tangu mwaka 2009, umbile la Kiyahudi na kampuni za kimataifa zimekuwa zikitoa matangazo mapya juu ya ugunduzi wa kiasi kikubwa cha gesi mashariki mwa Mediterania. Kwenye uwanja wa Tamar kilomita 80 magharibi mwa Haifa, futi za ujazo trilioni 9 za gesi inayoweza kutolewa iligunduliwa, kisha, miezi kadhaa baadaye, uwanja wa Dalit uligunduliwa magharibi mwa Palestina inayokaliwa kwa kati ilifikia futi za ujazo bilioni 500. Katika 2010 idadi iliyozidi mawazo iligunduliwa katika uwanja wa Jonathan magharibi mwa Palestina na futi za ujazo trilioni 16, Jarida la Sera ya Mambo ya nje la Amerika lilisema wakati huo, "Ni ugunduzi mkubwa zaidi wa gesi asilia ulimwenguni katika muongo mmoja."

d- Kwa hivyo, Uturuki imechukua hatua ya kuchukua na kununua meli ya kisasa na kubwa ya utafiti kutoka Korea Kusini, meli ya Al-Fatih, ambayo ilisafiri kwa mara ya kwanza mnamo 2011 na utafutaji wa mafuta na gesi ulianza. Halafu ulifuata mfululizo wa migogoro kati yake na Cyprus na Ugiriki kwa madai kwamba Uturuki ilikuwa ikichimba visima katika maeneo ya baharini ambayo ni milki ya Cyprus ya kipekee, na kisingizio cha Uturuki kilikuwa Wacyprus wa Kituruki na haki zao. Lakini, katika miezi ya hivi karibuni, Uturuki imeongeza kasi ya kazi ya utafiti baada ya kununua chombo kingine cha utafiti (uchimbaji wa pwani) kutoka Uingereza, ili kuwa na msururu wa vifaa vizuri vya uchimbaji baharini na meli za utafiti wa kijiolojia zinaweza kutafuta na kuchunguza kwa wakati mmoja katika Bahari Nyeusi, Pwani za magharibi ya Uturuki na kusini ya Cyprus katika mashariki mwa Mediterania.

Kwa hivyo, Uturuki ilihitaji kurekebisha hali yake ya kiuchumi kwa kukagua mafuta na gesi ... Labda inapaswa pia kutajwa kuwa uchumi wa Uturuki unakabiliwa na mapigo makubwa, maumivu ambayo yalionekana katika kuanguka kwa sarafu ya Kituruki, lira, ambayo ilimfanya Rais Erdogan kuongeza kasi ya utafutaji wa gesi kwa kutaraji kwamba atapata mwanga wa matumaini kwa uchumi huu, kwamba anaweza kudumisha umaarufu wake unaopungua kwa sababu ya kuanguka kwa lira na uasi wa viongozi wa chama chake dhidi yake na uundaji wa vyama vya upinzani ambavyo vinanyonyora umaarufu wa Erdogan. Kwa hivyo kazi ya utafiti wa Uturuki ilikuwa pana katika Bahari Nyeusi na haikufungika kwa maeneo inayozozania na Ugiriki katika Mediterania.

**2- Sababu za nje:**

a- Amerika inaunga mkono kuzinduliwa kwa juhudi hizi za Uturuki, kutoka pande mbili: Ya kwanza ni ya ndani: kwamba mtu wake nchini Uturuki, Erdogan, atakuwa katika nafasi nzuri ikiwa ataweza kuondoa vizuizi vya kiuchumi, kuongeza umaarufu wake na kuurudisha katika viwango vya juu kama ulivyokuwa kabla ya 2014, na hii inarahisisha utekelezaji wake wa sera za Amerika, kama vile kuingilia kati kwake Libya, ambapo anaweza kutumia katika hatua zake za kikanda kwa neema ya Amerika. Na ya pili: Amerika, wakati ambapo haitaki Ulaya iwe chini ya ushawishi wa kisiasa wa gesi ya Urusi, haitaki iwe huru katika suala la gesi. Ugiriki na Cyprus ni wanachama katika Muungano wa Ulaya na urefu wa mabomba unaanzia kutoka kwao hadi Ulaya, yote haya hayaipendezi Amerika, ndio sababu inaunga mkono tishio la uhuru wa Ulaya katika suala la gesi kupitia Uturuki. Kwa maana kwamba Rais wa Uturuki Erdogan anaitishia Ugiriki na kuchunguza kile inachokiona ni maeneo yake ya kipekee ya baharini bila makubaliano nayo kwa msaada fiche wa Amerika. Kwa hivyo, meli za jeshi la Amerika zilishiriki katika mazoezi ya kijeshi ya Kituruki. Wizara ya Ulinzi ya Uturuki ilitangaza ushiriki wa manuari ya USS Washington katika mazoezi hayo (Gazeti la Uturuki la Now, 26/8/2020),

Yote haya licha ya fedheha ya Amerika kuunga mkono nchi ndani ya muungano wake wa NATO dhidi ya nchi ya Ulaya, ambayo pia iko ndani ya NATO, na hiyo ilikuwa kwa badali ya ushiriki wa Ufaransa, ambayo pia ni kutoka nchi za NATO, katika harakati za kijeshi za Ugiriki, mienendo hiyo na baadhi ya uimarikaji wa kijeshi na sauti ya kukaidi ... yote haya yalisababisha hali ya hatari mashariki mwa Mediterania ambayo ilitishia kuzuka katika mapigano ya kijeshi kati ya nchi za NATO, ambayo ni kati ya Uturuki, ambayo inasaidiwa na Amerika kutoka nyuma ya pazia, na Ugiriki, ambayo inasaidiwa waziwazi

*Endelea... UK 15*

na Ufaransa, ikiwa jambo hili halikudhibitiwa baadaye.

b- Kwa upande mwingine, ruhusa ya Amerika ya mzozo mkubwa kutokea ambayo karibu ilibadilika kuwa hatua za kijeshi kati ya nchi mbili wanachama wa muungano wa NATO ambayo inaongoza bila kutupa uzito wake mzito wa kutatua mgogoro huo inaonyesha kujishughulisha kwake na shida zake za ndani kama vile virusi vya Korona na uchaguzi ... na kwamba kwa sasa imekabidhi hatua hii upande wa Ulaya, haswa Ugiriki, kwa Erdogan kwa msaada wake kwake kwa njia ambazo huzingatia fedheha ya Amerika kwamba Uturuki na Ugiriki ni wanachama wa NATO inayoongozwa na Amerika, na kwa hivyo Amerika ilishiriki pamoja na Uturuki katika mienendo ya kijeshi kama msaada kwa hali hizi. Kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine Pompeo alifanya ziara ya haraka huko Ugiriki, RT iliripoti "Pompeo alitoa wito kwa Uturuki kuondoa vikosi vyake kutoka Mashariki mwa Mediterania, ambapo meli ya utafiti ya Uturuki inayoungwa mkono na wahalifu wa jeshi inaendesha shughuli." (RT, 13/9/2020). Ikimaanisha kwamba Amerika, ambayo inaunga mkono Uturuki, ilijikuta mbele ya fedheha kubwa kutoka kwa washirika wake wa Ulaya, na ililazimika kumuagiza Rais Erdogan wa Uturuki kuondoa meli hiyo ya utafiti, ambapo ndilo lililofanyika, na kisha kuingia katika mazungumzo na majadiliano na Ugiriki, kwa sababu Ugiriki iliashiria sharti la mazungumzo hayo ni kuondolewa kwa meli ya kuchimba visima ya Kituruki.

**Tatu: Misimamo ya Nchi Nyengine:**

1- Msimamo wa Ufaransa ndio uliokuwa msimamo wenye nguvu zaidi wa Ulaya, kwani ilitangaza kutoka mwanzo kwamba imesimama na Ugiriki, na kutembea peke yake; Rais wake Macron alisema: ["Niliamua kuimarisha kwa muda uwepo wa jeshi la Ufaransa mashariki mwa Shirika la Kituruki la Anadolu, 13/8/2020)], na kisha kufanya mienendo pamoja ya majini na Ugiriki na kushiriki kwa ndege za Rafale ambazo ilizipelekwa nchini Cyprus, na kisha kufanya mienendo mingine mnamo 26/8/2020.

Iliihusisha Italy, pamoja na Ugiriki na Cyprus, ilifanya yote hata ingawa haina ushawishi katika eneo hilo! Yote hii inaonyesha kwamba inajaribu kujijengea tena ushawishi mkubwa. Kama ilivyo mienendo yake ya kijeshi pamoja na Ugiriki wakati ambapo Amerika inashiriki katika mienendo pamoja na Uturuki, hiyo inaleta changamoto fiche kwa Amerika, na kuihusisha kwake Italy nayo inaonyesha kwamba inasajili nchi za Ulaya pamoja nayo dhidi ya Uturuki, na vile vile mkutano ambao ilioufanya na baadhi ya nchi za Ulaya za Mediterrania (Italy, Malta na Uhispania pamoja na Ugiriki na Cyprus), na shinikizo lake ndani ya Muungano wa Ulaya na NATO kuchukua misimamo mikali dhidi ya Uturuki. [na Rais wa Ufaransa alisema: "Sisi kama Wazungu tunapaswa kuwa wazi na thabiti na serikali ya Rais Erdogan, ambayo leo inafanya tabia isiyokubalika ... na akaona kwamba "Uturuki sio mshirika tena katika eneo hili." (Ufaransa 24, 10/9/2020)]. Pia (Waziri wa Mambo ya nje wa Ufaransa Jean-Yves Le Drian alisema kuwa mkutano ujao wa Baraza la Ulaya umejitolea kuiadhibu Uturuki. Aliashiria kuwa Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan, anaendelea kukola moto na Ugiriki ili kuficha hali ngumu ya kiuchumi ya nchi yake. " (The Independent Arabia, 7/9/2020).

Licha ya ujasiri wa msimamo wa Kifaransa dhidi ya Uturuki na jaribio lake la kuvunja mfupa wa rais wa Uturuki, na licha ya ukweli kwamba Rais wa Uturuki Erdogan siye "Al-Fatih" wala "Qanuni" ambao majina yao hutumiwa kuzipa majina meli zake, na kwamba hakuifundisha Ufaransa somo katika Mediterania na wala angalau hakuzamisha meli yao yoyote, kwa adhabu ya maelfu ya maili ambayo meli na ndege zilisafiri kuvunja mfupa wake katika ua wa nyumba yake. Licha ya hayo yote, sera za Ufaransa zilibaki kuwa za uchakachuaji na zilikosa kina, huku Malta ikikimbilia kuukana muungano wake na Ufaransa. Waziri wa Mambo ya nje wa Malta, Evarist Bartolo alisema wakati wa mkutano na waandishi wa habari aliofanya na mwenzake wa Uturuki Mevlut Cavusoglu [Umoja wa Ulaya unapaswa kuutazama uhusiano wake na Uturuki kwa mtazamo wa kimkakati. Bartolo aliongeza: Nadhani wakati umefika kwa Muungano wa Ulaya kuishughulikia kwa uzito Uturuki, haswa katika biashara, haki za binadamu, na vita dhidi ya ugaidi. "(Shirika la Kituruki la Anadolu, 12/9/2020)].

2- Ama Uingereza, haikutoa maoni juu ya mvutano katika Mashariki ya Mediterania, ambapo iliongeza hofu ya Ufaransa. Badala yake, tangu Brexit, Ufaransa imekuwa ikiitazama kwa wasiwasi dori ya Uingereza, na wakati mwingine inagongana nayo, kama nchini Algeria. Na ikiwa masoko makubwa ya kifedha jijini London yataipa Uingereza nafasi katika masoko ya mafuta na gesi, haswa kwa bei kutokana na ushirika wake na mafuta ghafi ya Brent na bei inayofuata ya aina zingine za mafuta, na hata gesi asilia pia, Ufaransa, inayoiona Uingereza ikiachana na Muungano wa Ulaya, inajitafutia nafasi katika sekta hii muhimu ya kimataifa. Ndio sababu iliamua kujiasisisha nchini Ugiriki, labda itaisaidia kuwa mtendaji, sio mtumiaji pekee katika maswala ya nishati.

Kwa upande mwingine, Uingereza, wakati inaangalia kile kinachoonekana kama sera ya adhabu ya Muungano wa Ulaya dhidi yake kwa sababu ya kujiondoa kwake katika Muungano wa Ulaya, inatengeza njia yake na kuchora sera yake yenyewe, na labda iliogopa kuzuka kwa ghafla kwa taharuki katika mashariki mwa Mediterania, kwa hivyo haikuchukua misimamo dhidi ya Uturuki, kwani Ugiriki haina thamani yoyote kwa Uingereza ikilinganishwa na maslahi yake ya Kituruki. Na ni shabiki kipofu pekee kama Ufaransa ndiye anayeweza kupanda wimbi la Ugiriki! Kwa kulinganisha Uingereza na Ujerumani, Ufaransa haina maono yoyote, ambayo inaisababisha kurudi mikono mitupu baada ya vitendo vikali vya kisiasa ambavyo inavifanya. Kwa haya yote, rais wa Uturuki alimshambulia vikali, akisema: “Bw. Macron, utakuwa na matatizo zaidi na mimi binafsi. ”

*Endelea... UK 16*

Aliongeza: “Huna habari za kihistoria. Na wewe hujui historia ya Ufaransa, kwa hivyo usishughulike sana na Uturuki na watu wake "... (Al-Quds Al-Arabi, 12/9/2020).

3- Kwa upande wa Ujerumani, pia haikuteleza nyuma ya msimamo wa Ufaransa dhidi ya Uturuki, na ikatoa ofa ya upatanishi, wakati wengine walitafsiri kama ilicheza dori ambayo Washington ilipaswa kucheza. Iliendelea kujitenga na msimamo wa Ufaransa, kupatanisha na kutoa wito wa mazungumzo, na msimamo wake maarufu dhidi ya Uturuki ni kile Waziri wa Mambo ya nje wa Ujerumani, Heiko Maas, alichosema wakati wa ziara ya Athens ["Kuhusu utafiti wa Uturuki Mashariki mwa Meditterania, tuna msimamo wazi kabisa ... Sheria ya kimataifa lazima iheshimiwe. Kwa hivyo, maendeleo katika mahusiano ya Muungano wa Ulaya na Uturuki yatawezekana tu ikiwa Ankara itaacha uchochezi katika Mashariki mwa Mediterania… Utafiti wa Uturuki katika pwani ya Cyprus lazima ukome "(France 24 , 22/7/2020)].

4- Kwa upande wa Urusi, imejitolea kutumia uhusiano wake mzuri na Uturuki kupatanisha pande hizo mbili, lakini kama kawaida haiwezi kuchukua hatua yoyote, hata ikiwa ilitangaza mienendo ya kijeshi katika mashariki mwa Mediterania katika kujibu mienendo ya Ufaransa, na labda inataka kujikumbusha, [Urusi imepanga kuanza mazoezi ya kijeshi ya majini kwa risasi halisi katika Bahari ya Mediterania Jumanne ijayo, yenye kuendelea hadi Septemba 22, na nmengine kuanzia 17 hadi 25 Septemba, kulingana na Shirika la Bloomberg, ikinukuu Jeshi la Wanamaji la Uturuki, na msemaji wa Jeshi la Wanamaji la Urusi Igor Dygalo alisema, "Tuna uhusiano madhubuti wa kiuchumi na ulinzi na Uturuki. Lakini sera yetu ni kuzuia kuunga mkono upande wowote." Mienendo ya Urusi ilifuata mazoezi mengine ya kijeshi yaliyofanywa na Ufaransa katika eneo hilo, ambapo walipeleka ndege za kijeshi na manuari kusaidia Ugiriki na Cyprus katika mzozo huo. " (Independent Al-Arabiya, 7/9/2020)]. Hiyo ni kwamba, msimamo wa Urusi unabaki pambizoni, ukingojea ishara kutoka nyuma ya bahari, lakini inakumbusha nguvu yake.

**Nne:** Kwa yote yaliyotajwa hapo juu, mgogoro wa Uturuki na Ugiriki, ikiwa utarefushwa, utasababisha mpasuko mkubwa katika uhusiano wa kimataifa. Kuhusu uhusiano katika upande wa Atlantiki, nchi za Ulaya zinataka kuona nafasi yao katika ulimwengu ambao Amerika inajiondoa kutoka kwa uongozi wake kuelekea kulenga China na shida zake za ndani zinazoongezeka. Nchi hizi zinatafuta dori iliyotelekezwa na Amerika. Amerika chini ya utawala wa Trump haiachi kutishia maslahi ya Ulaya kwa kuwatumia wengine, kama dori za Urusi na Uturuki nchini Libya leo. Nchi za Ulaya zinaogopa sana kuwa mgogoro wa mashariki mwa Mediterania utasababisha kuharibu ndoto zao za chanzo salama cha gesi asilia iwapo Uturuki itadhibiti sehemu yake kubwa. Na kwa sababu Uturuki inaungwa mkono nyuma ya pazia na Washington, sera ya Ufaransa mashariki mwa Mediterania inajaribu kuzikataa dori ambazo yanatolewa Washington kwa Uturuki pamoja na Urusi.

Mzozo huu ndani ya atlantiki sio chini ya mzozo mwingine ndani ya Ulaya yenyewe. Msimamo wa Wajerumani ndio ulioizuia Ufaransa kushinikiza Ulaya iiadhibu Uturuki, ambayo ni kwamba haikufanikiwa kupata makubaliano ndani ya Muungano wa Ulaya dhidi ya Uturuki, kwa hivyo ilikwenda na kukusanya nchi za Mediterania za Ulaya! Ujerumani inafikiria mengi juu ya maslahi yake, na kwa kweli historia yake na Uturuki, ambapo Ujerumani na Dola la Uthmani zilipambana bega kwa bega dhidi ya washirika katika Vita vya Kwanza vya Ulimwengu, na mahusiano ya Ujerumani yalibaki imara na Uturuki, na kuchafuliwa tu na (uchokozi) wa Rais Erdogan na mara nyingi ukisukumwa na sera za Amerika. Hii ni ikiongezewa na jamii kubwa ya Kituruki iliyo nchini Ujerumani.

Ya tano: Iwapo mgogoro huu umekwisha au la, Uturuki imetangaza ugunduzi muhimu wa gesi katika Bahari Nyeusi, ambao ni jumla ya mita za ujazo bilioni 320, na hii inaisukuma katika utafiti zaidi katika Bahari Nyeusi na Mashariki mwa Mediterania. Jitihada za Uturuki za kupunguza mzigo wake wa kiuchumi zinaendelea, na uungwaji mkono wa Amerika kwa hilo unaendelea, ili kuihangaisha na kuishinikiza Ulaya, haswa Ufaransa, ili isiende mbali kupingana na kuvuruga sera ya Amerika katika eneo hilo!

Lakini inatia uchungu sana kwamba wakati wa karne iliyopita baada ya kuanguka kwa Khilafah, dola halisi ya Uislamu na chanzo cha utukufu wa Waislamu, nchi hizi zimekuwa mkia wa mataifa, hatma zao zikihadaiwa na wakoloni makafiri kwa zana zao, watawala katika nchi za Waislamu!! Walakini, alfajiri huzaliwa baada ya giza tororo la usiku, haswa kwa kuwa Hizb ut Tahrir inafanya kazi kuziregesha kama zilivyokuwa zenye kuvikwa taji, ushindi na nuru, Mwenyezi Mungu akipenda.

**إِنْ هُوَ إِلَّا ذِكْرٌ لِلْعَالَمِينَ * وَلَتَعْلَمُنَّ نَبَأَهُ بَعْدَ حِينٍ**

“Hayakuwa haya ila ni mawaidha kwa walimwengu wote * Na bila ya shaka mtajua khabari zake baada ya muda.” [Sad: 87-88]

**24 Safar Al-Khair 1442 H**
**11/10/2020 M**



Email: info@uqab.or.ke